# Mwongozo Wa Ulinzi Wa Data Kwa Biashara Ndogo Na Za Kati Nchini Kenya



Strathmore University

*Centre for Intellectual Property and Information Technology Law*

## Utangulizi

Bunge la Kenya lilipitisha Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act, 2019) ili kuuwezesha Haki ya Faragha kwa kila mja, kama ilivyo amrishwa katika Katiba ya Kenya 2010. Sheria hili lina lengo la kuhakikisha kuwa haki hii ya faragha kwa kila raia wa Kenya limelindwa. Hatua hii ni endeleo kubwa Kenya amabayo itahitaji mabadiliko makubwa katika shughuli za mashirika ya umma na ya kibinafsi.

## Data Binafsi/Nyeti

Data nyeti ni maelezo yanayo dhihirisha mambo kumhusu mtu kama vile kabila, hali ya afya, asili ya kijamii, imani, data ya biometriska, maelezo ya mali, hali ya ndoa, maelezo kuhusu familia kama majina ya watoto, wazazi, mwezi, na pia maelezo ya jinsia ya mtu binafsi.

**Lengo la mwongozo huu ni kukusaidia wewe kama mwenye biashara ndogo na za kati kuelewa majukumu yako ya kuhakikisha ulinzi wa data binafisi, kama ilivyoashiriwa kwenye Sheria ya Data Protection Act, 2019, unapoendeleza biashara yako.**

## Je, inakuhusu wewe?

Sheria hili linahusu kila biashara ndogo na ya kati inayokusanya, inayodhibitisha na inayoendeleza mchakato wa data binafsi kama sehemu kuu ya biashara yake. Hivyo basi, kama unakusanya, unadhibitisha au unaendeleza mchakato wa data binafsi, unapaswa kutii masharti ya sheria hili la ulinzi wa data.

- **Mtawala wa Data** huamua jinsi data binafsi hutumika na mbinu za kuendeleza mchakato wa data hiyo
- **Mchakataji wa data** hukusanya na kuchambua data binafsi kwa niaba ya mtawala wa data
- **Kamishna wa Data** huweka kizingiti cha chini cha usajili - ikiwa unazidi kizingiti, utahitaji kujiandikisha na ofisi ya Kamishna wa Ulinzi wa Data.

# Kanuni za kukusanya na kuchakata data binafsi

Sheria ya ulinzi wa data limepeana kanuni zifuatazo, na biashara ndogo na za kati zinapaswa kuzielewa na kuzitii kama zilivyoashiriwa.

## 01 Heshima kwa haki ya faragha

Unastahili kuheshimu haki ya kila mja ya faragha. Katiba la Kenya linasema kuwa faragha inajumuisha majukumu manne:

- Kutoendeleza utaftaji wa mtu au nyumba ya mtu yeyote;
- Kuto kuchukua na kushikilia mali ya wengine;
- Kijiepusha na kufichua au kuhitaji maelezo kuhusu familia au mambo ya kibinafsi ya mtu kuwasilishwa; au
- Kutokuingilia kati mawasiliano ya mtu

Kwa heshima ya data, Sheria ya Ulinzi wa Data linatekeleza haki hizi.

## 02 Sababu zilizo wazi na halali za ukusanyaji wa data

Ukusanyaji wa data binafsi inapaswa kufanywa kw njia zilizo wazi na sababu zake ziwe halali. Unafaa kuelezea dhahiri sababu za kukusanya, kudhibitisha na kuchakata data binafsi. Sheria ya Ulinzi wa Data linafafanua kuwa anayeathiriwa (data subject) ni yule ambaye data yake binafsi inakusanywa, inawekwa au inachakatwa.

## 03 Uchakataji ulio wa kisheria, halali na wazi

Unafaa kuhakikisha kuwa maelezo yote yanayohusiana na uchakataji na udhibiti wa data iliyokusanywa yanaweza patikana, wakati wowote. Maelezo haya lazima yawe wazi, yanayoeleweka kwa urahisi na yanayoweza kufikiwa yakiombwa.

## 04 Ukusanyaji na uchakataji wa data inayohitajika

Unapaswa kukusanya na kuchakata data inayohitajika pekee; hii ikiwa ni data muhimu inayohitajiwa kutekeleza majukumu yako kwa atakayeathiriwa na data iliyokusanywa na kuchakatwa. Uchakataji wa data binafsi unapaswa kuenedelezwa ndani ya vigezo vya sababu za ukusanyaji wake.

## 05 Data sahihi na ya kisasa

Unapaswa kuhakikisha kuwa data ulizokusanya ni sahihi na ya kisasa. Pale ambapo data si sahihi, atakayeathirirwa na matumizi ya data iliyokusanywa ana uhuru wa kuuliza data hiyo irekebishwe au ifutwe. Unapaswa kuirekebisha au kuifuta kulingana na ombi lao.

## 06 Muda wa kuziweka data zilizokusanywa na usalama wa data zilizohifadhiwa

Unapaswa kutupa data binafsi kwa njia nzuri na iliyo salama uchakataji ukikamilika, kwani haupaswi kuzishikilia kwa muda mrefu zaidi ya iliyokubalika. Pia unapaswa kumpa atakayeathirirwa na matumizi ya data binafsi maelezo kuhusu urefu wa muda unakusudia kuhifadhi data yake. Mwisho, unafaa kuhakikisha kuwa data binafsi zlizokusanywa zimewekwa salama.

## 07 Uhamisho wa data nje ya Kenya

Ikiwa unataka kuhamisha data binafsi nje ya Kenya, lazima uhakikishe kuwa misingi yote ya usalma yamefuatwa na anayepokea data hii/hizi. Misingi hizi za usalama lazima ziwe zinazofaa ili kuwezesha ulinzi wa data binafsi.Atakayeathirirwa na matumizi ya data iliyokusanywa pia anfaa kupewa maelezo kuhusu uhamisho huu na idhini yake kupeanwa ndiposa uhamisho wenyewe uwe halali. Idhini unaweza peanwa kwa maneno, kwa maandishi, kwa kudokezwa au kwa njia ya kielektroniki.

## Usajili wa Wadhibiti na Wachakataji

Sheria ya Ulinzi wa Data limeangazia kuwa kutakuwa na Ofisi la Kamishna wa Ulinzi wa Data, ambayo ni ofisi ya serikali. Kama wewe ni Mdhibiti au Mchakataji wa data, lazima usajiliwe na upewe leseni na Kamishna wa Ulinzi wa Data, ambaye atapeana vigezo vya kutimizwa vya usajili. Mara tu unapojiandikisha na kukidhi vigezo, unapata cheti ambacho kitahitaji kufanywa upya mara kwa mara.

## Ukusanyaji wa Data Binafsi

Sheria ya Ulinzi wa Data linahusika na ukusanyaji wa data binafsi; maelezo yanayo husiana na mtu asili. Ukusanyaji wa maelezo haya unaweza kuwa wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja. Pale amabapo, ukusanyaji wa moja kwa moja unashiria kuchukuliwa kwa maelezo kutoka kwa atakayeathiririrwa na matumizi ya data iliyokusanywa binafsi; na kwa upande mwingine, ukusanyaji usio wa moja kwa moja unaashiria kuchukuliwa kwa maelezo kutoka, kwa mfano, data ya umma, ambapo, atakayeathiririrwa na matumizi ya data iliyokusanywa amapeana idhini ya ukusanyaji wa maelezo yao binafsi kutoka mahali kwingine.

Pale ambapo mtu amepeana idhini ya ukusanyaji wa maelezo yake binafsi, unaruhusiwa kisheria kukusanya data kama hizo. Ikiwa hana uwezo wa kukubali ukusanyaji wa data zake za kibinafsi, kama ilivyo kwa mtoto, mlezi wake wa kisheria anaweza kupeana idhini kwa niaba yake.

## Ni nini haki za atakayeathirirwa na matumizi ya data iliyokusanywa?

Sheria ya ulinzi wa data linaashiria kuwa mathiriwa wa data iliyokusanywa ana haki zi-fuatazo:

### Haki ya kujulishwa jinsi data iliyochukuliwa inatumika

Unapokusanya data binafsi, ni lazima umuelezee anayeathiriwa na data hii mbona unaichukua na kuichakata data hiyo. Pia ni lazima umpee sababu zilizo wazi na halali za kukusanya na kuzichakata data yake.

### Haki ya kuweza kuifikia na kupata data iliyokusanywa

Mathiriwa wa data iliyokusanywa ana ruhusa na uhuru wa kuzifikia na kuzipata data zake binafsi zilizo katika umiliki wenyu wakati wowote, baada ya kuziitisha. Hivyo basi, unapaswa kuwezesha upatikanaji wa maelezo inayohitajika kwa kasi mwafaka.

### Haki ya kuweza kukataa uchakataji wa data zake zote binafsi

Atakayeathirirwa na matumizi ya data iliyokusanywa anaweza chagua kukuzuia na kukataa kuchakatwa kwa data zake binafsi. Hivyo basi, unahitajika kusimamisha uchakatiaji wowote haraka iwezekanavyo, kwani kuendeleza uchakataji utakuwa unafanywa bila ruhusa ya mathiriwa na litakuwa hatia.

### Haki ya kuuliza data zisizosahihi na za kupotosha zirekebishwe

Kulingana na maombi na maelekezo ya atakayeathirirwa na matumizi ya data iliyokusanywa, unapaswa kurekebisha na kusahihisha data zisizosahihi na za kupotosha. Marekebisho haya yanafaa kufanywa kwa upesi bila gharama kwa atakayeathirirwa na matumizi ya data iliyokusanywa.

### Haki ya kutaka data zilizo za uwongo na za kupotosha kufutwa

Unahitajika kufuta maelezo yasiyo kweli na ya kupotosha kumhusu atakayeathirirwa na matumizi ya data iliyokusanywa, kulingana na ombi lao. Kitendo hiki kitahitaji usahihishe data zote binafsi zilizo katika umiliki wenyu, mara kwa mara, ilikuepuka visa kama hivi.

## Wajibu wa Biashara Ndogo na za Kati Kutoa Arifa

Panapo wezekana, unapaswa kumweleza atakayeathiririwa na matumizi ya data iliyokusanywa yafuatayo:

- Haki zao kama zilivyo katika Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act, 2019)
- Kuwa data zao zinakusanywa na sababu za kufanya hivyo
- Watu wote, kando ya nyinyi wawili, ambao unakusudia kupitisha na kuhamisha data zao kwao na sababu za kufanya hivyo
- Anwani zako muhimu na majukwaa ya mawasiliano
- Maelezo ya kina kuhusu hatua zako za usalama zilizofanywa kulinda data iliyokusanywa.
- Aina ya data iliyokusanywa kwa hiari au iliyokusanywa kwa lazima kulingana na sheria
- Jinsi kuto kupeana sehemu yote au yoyote ya data iliyoombwa kunaweza mathiri atakayeathiririwa na matumizi ya data iliyokusanywa

Pale ambapo data binafsi zimefikiwa na kupatikana bila idhini (ukiukaji), unapaswa kumjulisha Kamishna wa Ulinzi wa Data kuhusu ukiukaji huu kwa maandishi, ndani ya masaa 72 ya ukiukaji huo kutokea. Baada ya masaa 72, unahitajika kuambatanisha arifu ya ukiukaji na sababu zinazoelezea ni kwa nini ulichelewa kupeana arifa.

## Tathmini ya Athari ya Ulinzi wa Data (Data Protection Impact Assessment (DPIA))

Pale ambapo uchakataji wa data ni hatari na kuna uwezekano mkubwa wa ukiukaji, unapaswa kutekeleza, ukishirikiana na Kamishna wa Ulinzi wa Data, Tathmini ya Athari ya Ulinzi wa Data. Hatua hii itaangalia an kuonyesha misingi zenyu zilizowekwa ili kulinda data binafsi.

Ofisi ya Kamishna wa Ulinzi wa Data utatatoa maagizo ya jinsi ya kufanya Tathmini ya Athari ya Ulinzi wa Data.

## Masharti ya Kuomba Ruhusa

Lazima uweze kudhibitisha kuwa atakayeathiririwa na matumizi ya data zilizokusanywa aliwapa idhini ya kukusanya na kuchakata data hizo binafsi. Sheria ya Ulinzi wa Data pia linaamrisha kuwa atakayeathiririwa na matumizi ya data iliyokusanywa anaweza kuondoa ridhaa yao wakati wowote, hivyo basi kuifanya uchakataji baada ya kuondoa ruhusa kuwa halali.

Ruhusa au idhini zinafaa kuitishwa kwa njia zisizotumia nguvu, hila, au ujanja. Njia zingine za kupata idhini zimetolewa katika Sheria ya Ulinzi wa Data.

## Data Binafsi zinazohusu Watoto

Pale ambapo atakayeathiririwa na matumizi ya data iliyokusanywa ni mtoto, idhini ya kuchukua na kuchakata data yake inafaa kupeanwa na mzazi au mlezi wake halali, kwani, mtoto hana uwezo wa kupeana idhini. Kama mtawala wa data au mchakataji wa data, unapaswa kuwa na namna za kupima na kujua umri wa atakayeathiririwa na matumizi ya data unayokusanya. Njia moja ya kufanya hivi ni kuitisha vitambulisho halali.

Lakini, hili si lazima kila wakati, kwa mfano, pale ambapo kunatolewa huduma za ushauri, wanaoendeleza kazi hii wanaweza pewa ruhusa ya kuchukua na kuchakata data binafsi za watoto bila idhini ya wazazi au walezi.

## Uchakataji wa Kiotomatiki

Unapoendeleza uchakataji wa data binafsi, hakikisha kuwa mchakato wote hujafanywa na programu, mifumo au zana za kiotomatiki pekee. Hakikisha kuwa sehemu ya mfumo wa uchakataji inajumuisha uamuzi wa kibinadamu, kwani Sheria ya Ulinzi wa Data linahitaji mifumo za kiotomatiki kujumuishwa na uamuzi wa kibinadamu. Hivyo basi, kwa jumla, mifumo zilizo za kiotimatiki pekee haziruhusiwi kuchakata data binafsi.

## Maafisa wa Ulinzi wa Data

Kulingana na uwezo wako, biashara ndogo na za kati zinaweza zingatia na kuchagua kuwa na Afisa wa Ulinzi wa Data (Data Protection Officer (DPO)), lakini si lazima, kulingana na Sheria ya Ulinzi wa Data. Kwa kuzingatia ugumu wa kulinda data, na kulingana na tasnia yako, unashauriwa kutafuta huduma za Afisa wa Ulinzi wa Data.

## Data zinazotumika kupata Faida

Ilikutumia data kupata faida, lazima atakayeathirirwa na matumizi ya data iliyokusanywa aidhinishe. Unahitajika kumueleza mathiriwa kwa uwazi sababu za kuataka kutumia data yake ili kupata faida. Baada ya maelezo hayo, lazima mathiriwa apeane idhini ya data yake kuchakatwa na kutumika kupata faida. Tendo hili la kutafuta faida kwa kutumia data linahitaji maelezo ya kibinafasi kama vile majina, anwani, nambari ya posta, nambari ya simu, au picha yasifichuliwe; kwani mathiriwa hapaswi kutambulika.

## Unaweza hamisha data binafsi nje ya Kenya lini?

Ili uweze kuhamisha data nje ya Kenya, lazima uthibitishie Ofisi ya Kamishna wa Ulinzi wa Data kuwa data ulizomiliki zimelindwa vilivyo. Pia, lazima uonyeshane sheria za kulinda data za atakayepokea data zinazohamishwa. Kamishna wa Ulinzi wa Data akiridhika, ataruhusu uhamisho wa data hizo.

## Sheria ya Ulinzi wa Data litatekelezwa vipi?

Atakayeathirirwa na matumizi ya data iliyokusanywa anaweza leta malalmishi dhidi ya mtawala na mchakataji wa data, pale ambapo amekosewa, kwa Kamishna wa Ulinzi wa Data. Baada ya kupokea malalamishi, Kamishna wa Ulinzi wa Data uanapaswa kuanza uchunguzi ndani ya siku 90. Pale ambapo Kamishna wa Ulinzi wa Data atapata ukiukaji wa Sheria , anweza kutoa ilani ya utekelezaji.

Baada ya uchunguzi zaidi, kukipatikana kosa au makosa, Kamishna wa Ulinzi wa Data anaweza kuwaadhibu wahusika kwa kuwapa faini ya shilingi milioni tano au asilimia moja ya mapato ya mchakataji au mtawala wa data, iliyo ya chini zaidi. Ikiwa mchakataji au mtawala wa data hajaridhika na adhabu aliyopewa, anweza peleka malalamishi yake katika Mahakama Kuu.

## Hitimisho

Kwa kuzingatia kuongezeka kwa umuhimi wa ulinzi wa data binafsi duniani na Kenya, Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act,2019) limetoa majukumu muhimu ambayo yatahakikisha haki ya faragha itatekelezwa. Ni muhimu kwa biashara ndogo na za kati kuzingatia na kufuata kanuni za sheria kila wakati, sana sana wanapochukua, na kuchakata data binafsi.

# WASILIANA NASI!

CIPIT ni kituo cha utafiti na mafunzo katika Chuo Kikuu cha Strathmore. Kijitabu hiki kimekusudiwa tu kama utangulizi wa kwanza wa Sheria ya Ulinzi wa Data - athari za Sheria hiyo ni pana, na haziwezi kufafanuliwa kikamilifu katika chapisho fupi. Tupo kukusaidia kuelewa sheria na jinsi inavyokuhusu. Tafadhali wasiliana nasi ikiwa una maswali yoyote juu ya kijitabu hiki, au tembelea wavuti wetu kwa maelezo zaidi.

+254 (0) 703 034 612 cipit@strathmore.edu

*Kijitabu hiki hakina ushauri kutoka kwa wakili. Ikiwa una swali kuhusu jambo maalum, tafadhali wasiliana na wakili wa ulinzi wa data au uwasiliane nasi.*

This study was made possible by a grant provided by the International Development Research Center (IDRC). We thank the organization for their continued support.

IDRC · CRDI
International Development Research Centre
Centre de recherches pour le développement international

Canada